**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**

Simu:+255 282515056/+255 685 304 646
E- mail: ps@ukerewedc.go.tz
Tovuti: www.ukerewedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,
1 Barabara ya Halmashauri,
33682 Bukongo,
S.L.P 41,
**UKEREWE/MWANZA.**

Unapojibu tafadhali taja:

---

Kumb Na. GA.25/95/01/112

14/03/2023

# TANGAZO LA NAFAZI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kupitia kibali cha ajira mbadala Kumb Na. **FA.170/359/01'B'/64** kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina tangaza nafasi saba (7) za kazi.

## WATENDAJI WA VIJIJI DARAJA LA III NAFASI TATU (3)

**1.0. Sifa za waombaji**

Awe amehitimu kidato cha IV au VI na mafunzo ya Astashahada/cheti cha Technician Certificate (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo – Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**2.0. Kazi za kufanya/majukumu.**

- Atakuwa mtendaji na mshauri wa serikali ya kijiji na kamati zake katika mipango ya maendeleo.
- Atakuwa Afisa masuuli na mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya kijiji.
- Atakuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- Atapaswa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo za Halmashauri ya kijiji.
- Atakuwa katibu wa kamati ya Halmashauri ya kijiji
- Ataongoza vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake
- Atapaswa kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na umasikini katika eneo lake.

- Atakuwa kiongozi wa wataalam waliopo ngazi ya kijiji.
- Atatekeleza majukumu yote kadri atakavyo kuwa anaelekezwa na msimamizi wake.

**3.0. Ngazi ya Mshahara**
Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mshahara serikalini yaani TGS B

## DEREVA II NAFASI MBILI (2)

**1.0 Sifa za waombaji**
Awe Amehitimu kidato cha IV au VI awe na Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisa ajali, awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

**2.0 Kazi za kufanya/majukumu.**
- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kufanya usafi wa gari
- Kuwapeleka watumishi mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kufanya shughuli nyingine kadri utakavyo elekezwa na msimamizi wake.

**3.0 Ngazi ya Mshahara**
Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mshahara serikalini yaani TGS B

## WASAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II NAFASI MBILI (2)

**1.0 Sifa za waombaji**
Mwombaji awe amehitimu kidato cha iv au vi na mwenye stashahada (NTA LEVEL 6) katika fani ya masjala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na mwenye ujuzi wa kompyuta.

**2.0 Kazi za kufanya/majukumu.**
- Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye regista *(incoming correspondence register).*
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi (*outgoing correspondence register)*
- Kusambaza majalada kwa watendaji *(action officers)*
- Kupokea majalada yanayorudi masjala toka kwa Watendaji
- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na Watendaji
- Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (*racks/filling cabinets*)au mahali pengine yanapohifadhiwa.
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi *(File tracking)*

**3.0 Ngazi ya Mshahara**

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mshahara serikalini yaani TGS C

**4.0 Masharti kwa ujumla**

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detail CV) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini wawili (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya vyeti vya kidato cha Nne au Sita pamoja na vyeti vya Taaluma na picha mbili za rangi za hivi karibuni.
- Testimonial, Provisional results, statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne (Form IV) na kidato cha sita (Form VI) havitakubalika.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (NECTA na NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostafishwa, waliofukuzwa kazi na kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Barua ya maombi iandikwe kwa mkono tofauti na hapo ombi lako halitapokelewa.
- Kichwa cha habari kitaje nafasi ya kada unayoomba kwa ufasaha
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi husika yatakataliwa.
- Waombaji watakao wasilisha taarifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.

Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Sekretarieti ya ajira na Halmashauri ya wilaya ya Ukerewe.

- Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kwa njia ya posta.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **29/03/2023** saa **9:30 alasiri.**
- **Aidha waombaji wote mnakumbushwa kupitisha nakala zenu za vyeti kwa kamishina wa viapo au wakili kwa ajili ya kuthibitishwa.**

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,
1Barabara ya Halmashauri,
33682 Bukongo,
S.L.P 41,

**UKEREWE/MWANZA.**

**Imetolewa na:**

Emmanuel L. Sherembi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**UKEREWE**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
UKEREWE

**Nakala:** Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe na kwenye tovuti (webite) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ambayo ni www.ukerewedc.go.tz. Na Sekretariet ajira.